



KUHUSU SISI

NPCC ni kituo cha Kitalaamu kilichoanzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Na 8 ya Mwaka 2016 ili kutoa huduma za udhibiti wa matukio ya sumu nchini.

WASILIANA NASI

0800112031 Masaa 24
022 222 1410 Muda wa Kazi

5 Barack Obama Drive
Dar Es Salaam

**MAMLAKA YA
MAABARA YA MKEMIA
MKUU WA SERIKALI
KITUO CHA TAIFA CHA
KUDHIBITI MATUKIO
YA SUMU**



HUDUMA YA KWANZA KWA ALIYEUMWA NA NYOKA

Endapo unatambua kuwa wewe mwenyewe au mtu mwingine ameumwa na nyoka fuata muongozo huu ili kujisaidia/ kumsaidia wakati taratibu za kumfikisha kwenye vituo vya afya unaendelea.

Dalili zinaweza kukusaidia kufahamu kama umeumwa na nyoka

- ✓ Majeraha mawili ya vidonda eneo alipouma nyoka
- ✓ Kuvimba eneo la jeraha na kubadilika rangi kuwa wekundu
- ✓ Kuhisi maumivu eneo la jeraha
- ✓ Wakati mwingine kupata shida ya upumuaji
- ✓ Kuhisi kichefuchefu na kutapika
- ✓ Kushindwa kuona vizuri
- ✓ Kutokwa na jasho pamoja mate

Huduma ya kwanza

- ✓ Weka kumbukumbu ya muda uliong'atwa / aliong'atwa
- ✓ Tulia/mtulize kiungo chenye jeraha kisitikisike (Mtikisiko husababisha sumu kusambaa kwa haraka mwilini)
- ✓ Ondoa nguo au mapambo yanayo bana kuzunguka eneo la jeraha sababu eneo la jeraha linaweza kuvimba.
- ✓ Mgonjwa asitembee, abebwe au asafirishwe kwa vyombo vya usafiri.
- ✓ Usipoteze muda kumtafuta au kumuua nyoka,

Mambo ambayo hutakiwi kuyafanya /kumfanyia aliyeumwa na nyoka

- ✓ Usifunge kuzunguka jeraha
- ✓ Usichanje au kukwangua eneo la jeraha.
- ✓ Usitumie barafu kukanda eneo la jeraha
- ✓ Usimpatie muhanga dawa yoyote pasipo na maelekezo ya daktari.
- ✓ Usielekeze eneo la jeraha zaidi ya usawa wa moyo wa muhanga.
- ✓ Usijaribu kunyonya sumu kwa mdomo.

Jinsi ya kuepuka kuumwa na nyoka

- ✓ Kujizuia kwenda maeneo yanayohisiwa kuwa ni makazi ya nyoka pamoja na kujaribu kuwakamata.
- ✓ Kujizuia kusogelea sehemu zinazohisiwa nyoka wanaweza kujificha kama vile; vichaka vya nyasi ndefu, mafukuto ya nyasi, mafukuto ya miti pamoja na mapango.
- ✓ Unapokutana na nyoka mpe nafasi ili aweze kukimbia, usijaribu kupambana naye
- ✓ Vaa viatu virefu (boots), suruali ndefu pamoja na vikinga mikono (gloves) za ngozi unapofanya kazi maeneo yanayohisiwa nyoka wanaweza kuwepo
- ✓ Epuka kutembea usiku hasa kipindi cha mvua, sababu ndicho kipindi ambacho nyoka huwepo maeneo ya wazi zaidi, ikilazimu kutembea chukua tahadhari.
- ✓ Tumia tochi unapotembea gizani

MUHIMU

Jambo kuu la muhimu kwa muhanga aliyeumwa na nyoka ni kutafuta kwa haraka iwezekanavyo msaada wa kitabibu hasa kwa kumfikisha kwenye vituo vya afya.

Baadhi ya Nyoka wenye Sumu Tanzania



Green Mamba



Koboko (Black Mamba)



kobra (Egyptian kobra)



Nyoka Miti (Boomsnake)



Kifutu (puffadder)



Spitting kobra (Cobra)

Usipoteze muda kumtafuta au kumuua nyoka, kama kuna uwezekano mpige picha.

Piga simu Kituo cha Kudhibiti Matukio ya Sumu kwa ushauri
0800112031 AU 022 211 3333